**MUHTASARI WA KIKAO KATI YA VIONGOZI WA DIASPORA MAREKANI NA WAJUMBE WA KAMATI YA MHE. RAIS YA KUTATHMINI UFANISI NA UTENDAJI KAZI WA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI – TAREHE 8 JUNI, 2023.**

## UTANGULIZI

Uongozi wa Jumuiya ya Watanzania New York na vitongoji vyake (NYTC) ulipokea mualiko wa maandishi kutoka Ubalozi wa Tanzania nchini Marekani na Mexico (Washington DC), na kutoka Uwakilishi wa Kudumu wa Tanzania katika Umoja wa Mataifa (New York), wa kukutana ili kutoa maoni ya wanadiaspora mbele ya Kamati ya Mheshimiwa Rais Dr. Samia Suluhu Hassan ya Kutathmini Ufanisi na Utendaji kazi wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, siku ya Alhamisi tarehe 8 Juni, 2023, saa kumi na mbili na nusu jioni, katika ukumbi wa Uwakilishi wa Tanzania Umoja wa Mataifa.

Agenda ya kikao ilikuwa ushirikiano baina ya wanadiaspora na Wizara, na mchango wa diaspora katika ujenzi wa diplomasia ya uchumi, pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hadidu rejea za Kamati.

## WALIOHUDHURIA

1) Mwenyeji wa Mkutano – Mhe. Balozi Hussein Kattanga, Mwakilishi wa Kudumu wa Tanzania katika Umoja wa Mataifa
2) Mwenyekiti wa Kamati – Mhe. Balozi Hassan Simba Yahya
3) Waheshimiwa Mabalozi wa zamani na Wajumbe wa Kamati waliofika
4) Naibu Mwakilishi wa Kudumu wa Tanzania, Umoja wa Mataifa – Mhe. Balozi Dr. Suleiman H. Suleiman
5) Wajumbe wa Sekretarieti ya Kamati
6) Viongozi Jumuiya ya Watanzania New York (NYTC), wakiwakilishwa na Mwenyekiti (Nathan Chiume), Katibu (Dr. Mwemezi Deusdedit) na Naibu Mhazini (Dr. Nyemo Mbennah)
7) Kiongozi wa Jumuiya ya Watanzania DMV (Pius Mutalemwa)
8) Kiongozi wa Jumuiya ya Watanzania North Carolina (Tony Ntirugeleza)
9) Kiongozi wa Jumuiya ya Tanzania Diaspora Hub (TDH), North Carolina (Nassor Basalama)
10) Wajumbe wa Bodi, Jumuiya ya DICOTA (Dr. Anicetus Temba; Dr. Mwemezi Deusdedit)

## MUHTASARI

Viongozi wa diaspora waliwakilisha maoni toka kwenye jumuia zao, na wajihitahidi kugawana hoja za kuongelea ili kuepuka marudio ya hoja kwa ajili ya kuokoa muda. Kwa ujumla, maoni yao yaligusia maeneo yafuatayo:

1) **<u>Hadhi Maalum (Special Status)</u>**

a. Wanadiaspora wengi wanasubiri tangazo rasmi la Hadhi Maalum ambalo Mhe. Waziri wa Mambo ya Nje, Dr. Stergomena Tax, ametamka litatolewa kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha, litakaloambatana na mabadiliko ya sheria mbalimbali yatakayorasimisha sera hii ili ianze kufanya kazi. Viongozi walipongeza Serikali kwa kuhitimisha mchakato wa sera hii mpya.

b. Japo wanadiaspora walitegemea kuona na kusoma *policy draft* ya Hadhi Maalum kabla ya kutangazwa rasmi, ili kufahamu kwa undani mawanda na mipaka ya maeneo 10 ambayo Wizara imeahidi yatakuwapo ndani yake, bado wana imani na kauli aliyoitoa Mhe. Rais mwaka jana ya kwamba maeneo hayo yatakidhi matarajio yao.

c. Vile vile, wanadiaspora wanasubiri kuona kama kutakuwa na *harmonization* kati ya Hadhi Maalum itakayotangazwa kwa diaspora, na haki za wananchi walio ndani ya Jumuiya wa Afrika Mashariki (EAC) ambao wananufaika na vipengele vya uraia pacha katika nchi zao, na pia kuongezeka kwa utengamano kupitia uhuru wa kutembeleana (*free movement*) ndani ya EAC.

2) **<u>Haki ya Uraia wa Kuzaliwa (Dual Citizenship)</u>**

a. Wanadiaspora wengine wangependa kuona katika mabadiliko yanayokuja ya **<u>kisheria</u> ya kupitisha Hadhi Maalum yakifuatiwa baadaye na yale ya kuruhusu haki ya uraia wa kuzaliwa (dual citizenship) yanawekwa ndani ya Katiba,** kupitia mchakato wa Katiba mpya ambao umeanza ***(i.e., an evolutionary approach towards constitutional dual citizenship right)***

**b.** Wanadiaspora wengine wanadhani ni vyema **mabadiliko yanayokuja ya <u>kisheria</u> ya Hadhi Maalum yatangazwe sambamba na yale ya <u>kisheria</u> ya kuruhusu haki ya uraia wa kuzaliwa (dual citizenship). Kwa maana nyingine, *a concurrent legal adoption of special status and dual citizenship*, ikiwa ni hatua ya awali kabla ya baadaye haki hii kuwekwa ndani ya Katiba Mpya kama "dual citizenship right".**

**c. Sababu kuu kwanini Wanadiaspora hao wangependa kuona "Haki ya Uraia wa Kuzawaliwa" inawekwa kwenye Katiba mpya, ni kuhakikisha haki hiyo inalindwa Kikatiba isiwe na nafasi ya kuondolewa na mabadiliko ya kisheria siku za mbeleni.**

d. Viongozi walisisitiza Tanzania ina hatari ya kuendelea kupoteza nguvu kazi (*human capital)* ya wanadiaspora wake duniani, hasa wale wenye ujuzi na maarifa ya juu katika fani zinavyohitajika na nchi nyingi, kama sayansi, technolojia, nyuklia, *artificial intelligence, data, space and aeronautics*. Wanadiaspora wenye ujuzi huu wanapewa uraia wa nchi zingine zinazowahitaji, hivyo Tanzania inaendelea kuwakosa katika kuleta maendeleo ya Tanzania kama haitakuwa na utaratibu wa kuhakikisha wanarudi nyumbani.

e. Viongozi walishauri mjadala wa kisera usilenge kuwa wa kuchagua kati ya Hadhi Maalum au Dual citizenship *(yaani "either or" debate)*, kwavile kuna viashiria vingi vinavyoonyesha ya kwamba sera zote mbili zitahitajika na zitalinufaisha taifa la Tanzania na wanadiaspora wake, hata kama itabidi kuanza kutumika sera moja itakayofuatiwa na nyingine ukifika muda muafaka.

f. Badala yake, viongozi walishauri ufanyike utafiti wa kisayansi wa kuelewa diaspora ya Watanzania huko walipo wanaishi katika mazingira gani ya kisheria ili kujua jinsi sheria hizo zinavyowabana au kuwaruhusu iwapo sera mojawapo itaamuliwa na Tanzania. Utafiti utasaidia utungaji wa sera kulingana na uhalisia wa maisha ya wanadiaspora; kuelewa tofauti za sheria baina ya nchi na nchi; na kujua tofauti za mahitaji, malengo na matarajio yao kimaisha ili kutunga sera kamilifu zitakazowagusa wanadiaspora wote.
g. Mifano kadhaa ilitolewa, ikiwamo baadhi ya nchi kama Omani ambayo diaspora aliyechukua uraia wa nchi hiyo anaweza kupoteza uraia huo iwapo atachukua uraia wa nchi nyingine. Vile vile, Watanzania waliochukua uraia wa Marekani na wameajiriwa na Serikali ya Marekani katika zile ajira ambazo lazima uwe raia wa Marekani, wao hawaruhusiwi kuchukua uraia wa nchi nyingine, n.k.

**3) <u>Mawasiliano kati ya Balozi zetu Marekani na Jumuiya za Wanadiaspora</u>**

a. Viongozi walishauri kwamba ili kuboresha ushirikiano na upashanaji habari, ni vyema taarifa muhimu kutoka Wizarani zifikie Balozi zetu kwa wakati na kwa muda muafaka, ili kuwezesha viongozi wa diaspora (na wanadiaspora kwa ujumla) kupata muda wa kuhudhuria mialiko, kupanga shughuli au sherehe za pamoja za kitaifa, au kujiandaa na ujio wa Viongozi kutoka nyumbani.
b. Viongozi walisisitiza umuhimu wa kujenga kuaminiana kati ya Wizara na Ubalozi kwa upande mmoja, na viongozi wa diaspora na wanadiaspora kwa upande mwingine.
c. Viongozi walieleza kwamba sababu iliyopelekea baadhi ya wanadiaspora kuwa na mashaka na Hadhi Maalum ni kutokana na ukosefu wa taarifa za kina kutoka Wizarani, na kutokutimizwa kwa ahadi ya kuonyeshwa draft ya policy hii, hali iliyopelekea kujengeka kwa hofu, zingine zikiwa za kusadikika.
d. Viongozi walishauri uundwaji wa ***Diaspora Council*** kupitia sera mpya ya diaspora, itakayoundwa na Wizara pamoja na viongozi wa diaspora, ambayo pamoja na mambo mengine, ifanye mikutano ya mara kwa mara, yaani ***Diaspora Conferences***, kujadili namna ya kukuza ushirikiano na ushiriki wa wanadiaspora nchini Tanzania.

**4) <u>Huduma kwa Wanadiaspora kupitia Balozi zetu</u>**

a. Balozi zetu ziendelee kupeleka **huduma za pasipoti** katika kona zote za nchi ya Marekani, kwa kufanya miadi na wanadiaspora wanaohitaji huduma hizo kila mara, hasa wale walio mbali na vituo vya Washington DC na New York.
b. Wanadiaspora wa Marekani wanaendelea kusubiri mrejesho kutoka Wizarani kuhusu "pilot study" iliyofanyika mwisho wa mwaka jana 2022 ya kutoa huduma ya kadi za NIDA. Wanadiaspora ambao bado wana uraia wa Tanzania wanasubiri kwa hamu kuweza kupata **huduma za NIDA** wakiwa ughaibuni.
c. Wanadiaspora wenye uraia wa Tanzania wangependa kuhesabiwa katika **Sensa ya watu na makazi** zinazofanyika Tanzania. Wangependa Serikali ilianze kujipanga sasa kwa ajili ya kuwahesabu wanadiaspora kwenye Sensa ijayo.
d. Wanadiaspora wenye uraia wa Tanzania wangependa **kuandikishwa na kuweza kupiga kura katika uchaguzi mkuu ujao wa 2025 wakiwa ughaibuni**.
e. Viongozi walishauri Wizara na Balozi zetu kufanya "marketing promotion" na "communication strategy" ya kuelezea faida na umuhimu wa wanadiaspora kujisajili katika ***Diaspora Data Hub*** iliyozinduliwa majuzi. Hii itasaidia kuendelea

kujenga imani kwamba Hub hii ina manufaa ya kiuchumi na itawawezesha wanadiaspora kupata huduma bora za kiserikali na kibiashara kutoka nyumbani.

5) **Kubadili Sheria za Fedha za Benki Kuu na kuondoa Urasimu wa Kibiashara**

a. Ili kuleta mafanikio ya diplomasia ya uchumi, viongozi wa diaspora walishauri sheria mbalimbali za Fedha zinazoendesha Benki Kuu ya Tanzania (BoT) zifanyiwe marekebisho ili ziendane na kasi na namna mpya za kutuma malipo, kutumiwa malipo, na kufanya miamala ya fedha duniani.
b. Uwezo na ushiriki wa diaspora katika uchumi wa Tanzania ni mpana zaidi kuliko kwenye eneo la ***remittances*** ambalo wengi hulizungumzia. Sera mbalimbali zifanyiwe marekebisho ili kuwezesha diaspora ***kuwekeza, kuweka akiba, kukopa, na kufanya malipo*** kwa uwazi na urahisi zaidi nchini Tanzania.
c. Hata hivyo, kuondoa urasimu na kushusha gharama za kutuma na kupokea fedha za kigeni, utaongeza *remittance*s za fedha kwa wingi zaidi nchini Tanzania kutoka diaspora, kama tunavyoshuhudia kwa baadhi ya majirani zetu walikwishaondoa vikwazo hivyo.
d. Wanadiaspora wanahitaji kushirikishwa zaidi kwenye kununua hisa katika masoko ya mitaji, na dhamana za Serikali (treasury bonds), na kupata riba (interest rates) stahiki za kukopa na kuweka akiba katika Benki za nyumbani.
e. Serikali izipe wajibu wa lazima mabenki yote nchini Tanzania kutengeneza bidhaa (banking products) za diaspora, ili ziweze kuwa na ushindani na zenye huduma bora zaidi kuliko hivi sasa.
f. Vile vile, taasisi kama za mabenki zipewe ruhusa ya kutazama takwimu (data) kwenye *Diaspora Data Hub* ili kuweza kutengeneza bidhaa na huduma zinazokidhi haja na uwezo wa wana wanadiaspora.
g. Wanadiaspora waweze kuunganisha akaunti za benki zao za Tanzania na zile za nje na kufanya mialama kwa urahisi na kwa gharama sawa au nafuu.
h. Kuwezesha masharti ya kukopa kwenye benki za Tanzania kwa kutumia ajira za ughaibuni au pensheni za nje ili kununua nyumba, kuanzisha biashara n.k.
i. Kuendelea kuondoa urasimu katika maeneo mbali mbali yanayokwamisha kufungua na kuendesha biashara Tanzania, na kuwezesha kupata huduma za kiserikali ukiwa nje ya nchi kwa ufanisi zaidi. Kwa mfano – kuwezesha kuhakiki ujuzi, elimu na uzoefu wa watoa huduma walioandikishwa katika tovuti za Serikali kwa kuona vyeti vyao mitandaoni.
j. Kuondoa vikwazo vya anuani za makaazi kama sharti la ufunguzi na kufanya biashara Tanzania.
k. Kuondoa masharti ya kodi kama VAT kwa biashara mpya kulipa kodi kabla ya kupata mapato, jambo ambalo linalowaathiri wanadiaspora na Watanzania wengi wanaoanzisha biashara mpya Tanzania.

6) **Kubadili Sera na Muundo wa Wizara**

a. Viongozi wa diaspora walishauri kwamba Sera mpya ya Mambo ya Nje iendane na mabadiliko ya geographia ya kisiasa duniani, kwa kutambua kukua kwa nguvu ya China, umuhimu wa ukanda wa bahari ya Pacific katika siku zijazo, n.k.
b. Vile vile, sera mpya izingatie umuhimu wa madini ya kutengeneza betri za magari ya umeme, na uchumi wa nishati za mafuta na gesi ambazo zote tunazo, na zinaenda kubadili utizamo wa Taifa letu duniani katika siku za mbele.

c. Viongozi walishauri mapitio ya sera yetu ya mambo ya nje iliyotupa heshima toka uhuru, ili isipoteze umuhimu wakati wa utekelezaji wa sera mpya ya diplomasia ya uchumi.
d. Viongozi walishauri ili kufanikisha sera ya diplomasia ya uchumi, ni muhimu kuajiri wataalamu wa fedha na biashara ya kimataifa katika Wizara na Balozi zetu, badala ya kuwa na wanadiplomasia wasio na ujuzi wa kina wa maeneo haya.
e. Wizara iwe na mkakati endelevu wa kuhakikisha Watanzania na wanadiaspora wanachukua nafasi za ajira katika mashirika makubwa ya kimataifa, na kujaza *quota* za ajira ambazo tunapewa.
f. Wizara itengeneze mkakati wa kuwatumia wanadiaspora kutafuta na kupeleka wawekezaji nchini Tanzania.
g. Wizara ibadilishe muundo wa Idara zake kwa kuzigawanya kufuatana na *functions* (maudhui) chini ya Idara Kuu au *Bureau*, na kugawa Idara kubwa kama "Asia na Australia" au "Europe na America" ili ziendane na mabadiliko ya kisiasa duniani.
h. Wizara itazame uwezekano wa kufungua *Consulates* nyingi zaidi (hasa katika nchi kubwa kama Marekani, China na India) ili kupanua huduma. Vile vile, kufungua Consulates katika miji muhimu vya kibiashara kama Lubumbashi, Accra na Cape Town.
i. Vile vile, Wizara ifungue *Commercial Offices* au *Trade Missions* kwenye Balozi zake ili kuongeza nguvu ya kuvutia uwekezaji, biashara na utalii.
j. Mwisho, ili kukuza diplomasia ya utamaduni na lugha ya Kiswahili, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Elimu na ile ya Utamaduni, ianzishe Taasisi ya Kiswahili (***Kiswahili Institutes***) na kufungua dawati au ofisi zake kwenye Balozi zetu nje ya nchi.

Kikao kilifungwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Mhe. Rais majira ya saa tatu ya usiku.

**IMETAYARISHWA NA:**

**NATHAN CHIUME**

**MWENYEKITI, EXECUTIVE COMMITTEE**
**NEW YORK TANZANIAN COMMUNITY (NYTC).**
**13 JUNI, 2023.**